Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 79 No. 208 | MUHAR-SAFF 1440 AH | NOVEMBA 1-15 2019 | TABOOK 1398 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na husema wale waliokufuru: Mbona hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake? Hakika wewe ni Mwonyaji; na kila kaumu ina Kiongozi
AR-RA'D 13:8

Ni Kweli Jalsa Salana ya Miaka 50

Na **Khamis Wamwera**



Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Alhamdulillah, ninamshukuru Allah subhana wataala kwa kuifanya Jalsa Salana yetu ya miaka 50 kuwa ya neema na fadhila kubwa sana. Tuliianza kwa kheri na salama na kukhitimisha kwa amani. Kwa nini nisimshukuru Allah? Kwa mara nyingine tena nasema Alhamdulillahi Rabbil-alamin.

Pamoja na hayo, binafsi nimeshindwa kuvumilia kukiweka kile nilichonacho moyoni ila kukiweka hapa hadharani. Nakiweka mbele ya wasomaji kile nilichokiona kwa mboni yangu. Kwayo huenda haya yakasaidia kuonyesha taswira ya Jalsa Salana yetu mwaka huu.

Tangu tarehe 27 Ijumaa hadi tarehe 29 ya mwezi Septemba 2019, Wanajumuiya toka janibu mbalimbali ya Tanzania walifika kwenye Jalsa ya mwaka huu. Ndugu zetu wapatao 12 toka Uganda waliungana nasi. Wanajumuiya kutoka Kenya, Msumbiji na Malawi pia walihudhuria kule Kitonga mjini Dar es salaam. Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani kutoka Pakistan ndiye alihudhuria kwa ruhusa ya Khalifa mtukufu. Jalsa Salana hii ya nusu karne ilihudhuriwa na watu takriban elfu saba kasoro kidogo, ni watu 6,993 hivi. Si idadi ndogo, ni kubwa. Mimi niliona kama muujiza machoni pangu. Ninasema muujiza kwa sababu Jalsa Salana ya kwanza iliyofanyika Masjid Salaam mnamo mwaka 1969, kwa kweli ni mbali mno na hii. Sikumbuki idadi yetu tulikuwa wangapi, lakini hata hivyo hatukuweza kujaza msikiti wa wakati ule.

Jalsa Salana ya mwaka huu imetia fora sana. Huba na mapenzi yalitanda kwa kila mwanajumuiya. Kila mmoja akutanapo na mwenzie wanaombeana salama na amani kwa maamkizi ya Kiislamu. Kila sura ya mwanajumuiya ilionekana ya bashasha na tabasamu tele. Ni udugu uliokomazwa na malezi mema ya Kiislam. Jalsa Salana hii ya kufikisha miaka 50 kwa kweli ilisisimua sana jasadi yangu nikajiona kana kwamba ni mwanajumuiya mpya mwenye ari na jazba tele.

MAMBO UKUMBINI

Sasa tunaingia kwenye ukumbi ambako Jalsa Salana inafanyika. Hapa ni Jalsa Gah. Watu wote

Mahafali ya Ahmadiyya Sekondari Yafana

Na **Pazi Mazongera**

Kwa fadhila za Allah Mtukufu shule ya sekondari ya Ahmadiyya iliyopo Kitonga nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam ilifanya mahafali yake ya 6 kwa ajili ya wahitimu wa kidato cha nne. Mahafali hayo ya aina yake na yaliyodhuriwa na wageni mbalimbali pamoja na wazazi walioongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmood Chaundry sahib.

Akitoa maelezo ya awali kwa mgeni rasmi, meneja wa shule Mussa Mgeleka sahib alimueleza Amir Jamaat kuwa mahafali haya yana wahitimu 54 ambapo idadi hii ni kubwa toka Shule ianzishwe. Idadi hii imeongezeka, kwa Shule ndani ya miaka minne ya wanafunzi hawa kumefanyika maendeleo makubwa ya Miundo mbinu, taaluma na utumishi hivyo kuboresha mazingira ya kuishi wanafunzi na kufundishia, Alieleza meneja wa shule.

Ujenzi wa Maabara na Vifaa vyake na Maktaba yenye vitabu, ilipelekea kuongeza huduma ya kujifunzia kupanuka na hata kwenye mtihani wa Shule binafsi kanda ya Ukonga, Mwanafunzi wa kwanza na bora ametoka katika Shule yetu ya Ahmadiyya Secondary. Vile vile Ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Shule na Taaluma na Ofisi za Walimu umefanyika na kupelekea kuongeza tija kwa ufundishaji na usalama wa mitihani na usimamizi wake.

Mengine ni pamoja na ujenzi wa Mabweni mapya ya wasichana ambayo yanahuduma kwa ndani

Endelea uk. 9

Kwa Njia Hii Tutakuwa Tumemuenzi Mwl Nyerere

Na **Rajabu Abasi Mkieti**
Ikwiriri, Rufiji

Siku ya tarehe 14 october kila mwaka katika nchi yetu, ni siku muhimu sana kwa kila mtu yoyote yule mpenda maendeleo,mwanaharakati au mzalendo wa Taifa hili na hata rafiki wa Taifa hili.Kwani kwa mwaka huu itakuwa ni miaka ishirini tangia kufarika kwa Baba wa taifa hili. Sherehe mbalimbali kama njia ya kumbukizi ya mwanafalsa,mtu aliyekubali kujisahihisha hata alipokosea mtu aliyejitolea maisha yake kwajili ya kutetea nchi yake na bara zima la Afrika, huyu si mwingine bali ni Mwl Julius k. Nyerere. Kuna swali moja la kujiuliza kwanini kila mwaka tunaandaa makongamano, mijadala ya kitaaluma na mihadhara ya kisomi kama njia ya kumkumbuka mpiganaji huyu wa Taifa hili? jibu lake linaweza kuwa hii ndio njia ya kumuenzi na kuzirithisha athari zake kwa vizazi vya leo na kesho katika Taifa hili. Kwangu mimi naweza kuona kuwa hiyo ni sehemu ndogo sana katika kumkumbuka Baba wa Taifa hili Mwl J.K Nyerere. Kama tukitafakari kidogo tunaweza kugundua kuwa tuna ombwe kubwa katika kumuenzi Mwl Nyerere, kwani katika hali ya mijadala na mihadhara ni sehemu ndogo sana ambayo itakuwa ni kurejea baadhi ya vifungu vya maandishi na semi zake ila sehemu kubwa tumeiacha bila kuifanyia kazi. Wakati nikipita katika maadishi mbalimbali ili kutaka kumjua mtu huyu ambaye wakati anafariki nilikua ndio ninaanza darasa la kwanza nami nikagundua kuwa hata wanahistoria wetu wamekumbwa na tatizo la

Endelea uk. 9

Matumizi Sahihi na Bora ya Mitandao uk. 8

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Jenga Hoja, Usihamaki!

Raisi mstaafu wa awamu wa nne, Dr Jakaya Mrisho Kikwete ametoa wito kwa watanzania kujenga utamaduni wa kujenga hoja na kujiepusha kuhamaki. Onyo hilo amelitoa katika chuo cha Mwalimu Nyerere Kivukoni katika kumbukizi ya miaka ishirini toka Mwalimu Nyerere atutoke.

Dr Kikwete katika kufafanua hoja yake alitoa kisa cha marafiki wawili waliosoma pamoja shule ya wavulana Tabora. Julius Kambarage Nyerere na Kaluta Amri Abedi walikuwa ni wanafunzi wa Tabora na walipendelea kuzungumzia masuala ya dini. Siku moja Kaluta Amri Abedi alibeba Qur'an Tukufu na akaenda kwa Julius Kambarage Nyerere kuzungumzia juu ya utatu mtakatifu. Kabla hata mazungumzo hayajaanza Julius Nyerere akahamaki. Kaluta Amri Abedi taratibu alikusanya vitabu vyake na kumwambia mimi nikadhani una hoja kumbe ni kuhamaki, mimi naondoka.

Tukio hili Dr kikwete anasema mwalim Nyerere alilielezea kwenye NEC, akiwaelezea wajumbe umuhimu wa kujenga hoja.

Itakumbukwa dhana ya kujenga hoja ya Mwalim Nyerere ameambiwa mara mbili na Waahmadiyya. Kwanza ni hiyo hapo na nyingine imeelezwa katika kitabu cha **Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya.** Katika kitabu hicho tunaelezwa jinsi Sheikh Mubarak Ahmad mbashiri wa kwanza kutumwa Afrika mashariki alivyopewa nafasi kufundisha Dini ya Islam shuleni hapo. Kati ya moja ya somo alieleza kuwa hata Biblia imekatazwa ulaji wa nyama ya nguruwe. Jambo hili lilizua vuta ni kuvute miongoni mwa wanafunzi, Wakristo walisisitiza kuwa habari hiyo haina chembe ya ukweli. Mmoja wa waliokuja juu kama moto wa kifuu ni Julius Kambarage Nyerere kumuona tu Sheikh Mubarak Ahmad huku ana hamaki akataka habari za nguruwe katika Biblia. Sheikh Mubarak alimtuliza na kumuambia msomi hatakiwi kuhamaki na kuyumbishwa na jazba anachotakiwa ni kujenga hoja. Baada ya maneno hayo alimuonesha Julius Kambarage Nyerere nukuu inayoelezea kukatazwa ulaji wa nyama ya nguruwe, Julius Kambarage Nyerere alijisikia vibaya sana na akaamua kusoma kwa bidii na kujitahidi kujenga hoja. Historia ya baadaye ya maisha yake inaonesha athari za tukio hilo Nyerere alitokea kuwa muongeaji mzuri katika mihadhara pale shuleni hata alipokuwa Makerere.

Jabari la Mahubiri Limetutoka

Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu

Amma baadu, kwa fadhili za Allah nimesoma makala ya bwana Rajabu Abasi Mkieti kuhusu kichwa cha habari hapo juu, kwa kwelii kimenivutia sana. Nami nimeona niongeze habari ambayo ni muhimu sana aliokutana nayo marehemu katika harakati zake za mahubiri, habari ambazo zinasikitisha kidogo.

Mimi kwa mara ya kwanza nilikutana na marehemu msikitnji Tabora alipokjuwa amekuja kumuona Bi Rehema bint Abdallah Witika wa Igoko, Tabora. Kama kawaida ya Waahmadiyya tulikumbatiana kana kwamba tulifahamiana muda mrefu. Baada ya kupata utambulisho kutoka kwa marehemu Mwalimu Abdallah Salehe nilifarijika sana, kwa hiyo tulipomaliza kusali sala ya Magharibi nikamchukua marehemu pamoja na mke wake nikawapeleka nyumbani kwangu Shede Railway Quarters. Mke wangu aliwapokea vizuri sana na haraka tukawaandalia wageni chakula.

Mwaka uliofuata nilipata likizo ya siku 28 nikaondoka na familia yangu kwenda kupumzika nyumbani Tanga.

Siku ya Ijumaa nilifika msikitini Tanga na kwa mara nyingine tukaonana na marehemu na baada ya sala akanipeleka nyumbani kwake mtaa wa mwanzange. Tulipata muda mrefu wa maongezi hasa katika harakati zake za kutafuta ukweli uko wapi. Aliniambia kwamba wakati anajifunza kazi ya kushona viatu bosi wake Singasinga alimpeleka hekaluni kwao ili ajifunze dini yao. Baadaye akaenda kwa Wakristo akaanzia na dhehebu la Anglikana kisha akahamia dhehebu la Katoliki. Kule kanisani kwa Wakatoliki akakutana na Baba Mchungaji Odilo na akajitambulisha kwamba yeye ni Muislam lakini anataka kujua mafundisho ya dini ya Kikiristo ili aweze kujiunga nayo iwapo atapata ukweli. Baba Mchungaji Odilo akaanza mafunzo ya msingi kwa muda wa wiki moja halafu akanikabidhi kwa mwalimu mwingine Sister Scollast Msoffe.

Marehemu shughuli zake za ushonaji ni barabara 15 au jina maarufu la mtaa BOMBOKA. Pale mtaani ilitokea Sheikh mmoja wa Kisuni alijiunga na Ahmadiyya ikawa patashika nguo kuchanika na Masheikh wenzake ile hali ikampa hamasa marehemu kutaka kujua kulikoni, ndipo yule Sheikh akamjulisha kuwa kama anataka kujua ukweli uko wapi basi ajiunge na Ahmadiyya. Marehemu alipelekwa msikiti wa Ahmadiyya hapo akakutana na Sheikh AbuTwalib Sandi. Tukumbuke muda wote huo bado alikuwa anaendelea na darasa lake kule kanisani.

Marehemu alijiunga na Ahmadiyya baada ya kutosheka kabisa kwamba ukweli upo kwa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya.

Siku moja mwalimu wake Sister Scollast alikwenda kumtembelea mwanafunzi wake pale barabara ya 15 akakuta watu wengi wamemzunguka wakati akitoa maelezo ya falsafa ya YESU kuumba ndege, wakati huo huo Baba Mchungaji Odilo naye akatokea akiwa na nia ya kumtembelea mwanafunzi wake. Akasikiliza kwa makini maelezo ya marehemu, hapo ndipo alipoondoka haraka kurudi kanisani. Sister aliporudi Baba Mchungaji alimuita na kumueleza kwamba kuanzia leo yule mwanafunzi usimfundishe tena.

Sister Scollast akaanza kuathirika na mahubiri ya Mzee Abasi Mmkieti ikawa mara kwa mara anatoroka kanisani na kwenda barabara ya 15 kumbe Mchungaji Odilo anafuatilia mwenendo wake.

Masikini mahubiri ya Mzee Abasi Mkieti yamponza Sister Scollast kwani baada ya Baba Mchungaji Odilo kubaini kwamba Sister hana mapenzi tena nakaziza Usister. Hapo akapanga mpango kazi na Sister Scollast akauwawa kinyama kwa kukatwa katwa viungo vyake hadi kifo – Innalillah wainnailaihi rajiuun.

Abdallah Mambo Mshenga
Garincha - Darwesh

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Lajna wa Kusini mwa Jangwa la Sahara Wakutana

Na Pazi Mazongera

Khalifatul Masih V, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad atba alitoa maelekezo kwa mkuu wa kitengo cha Lajna Immaillah kule Markaz, Rihana Ahmad sahibat aje ukanda wa Afrika Mashariki na kuendesha mafunzo rejea ya kiuongozi ambayo yalifanyika tarehe13 hadi 15 mwezi sepetemba, 2019. Mkutano huo kihistoria ulihusisha nchi za Kenya, Uganda, Malawi, Zimbabwe na Tanzania ambayo ilikuwa mwenyeji wa mkutano huo. Mkutano huo wenye manufaa na faida nyingi kwa Tanzeem ya Lajna Imaillah ulifanyika katika msikiti mpya wa kisasa wa Masjid Salaam, uliopo mjini Dar es Salaam. Lilikuwa ni tamasha kubwa la kidini lilizongumizia mambo mengi kwa uchache walikumbushana juu ya Imani za Masih Aliyeahidiwa, thamani na umuhimu wa kiapo cha Lajna Imaillah, uzuri na majukumu ya Lajna Imaillah, mwanzo wa historia ya Lajna Imaillah, katiba na miongozo ya Lajna Imaillah, sababu na madhumuni ya kuanzishwa kwa Lajna Imaillah, kanuni za Majlis shura ya Lajna Imaillah, baraka za kujitolea mali, namna bora ya kufunga hesabu za mwezi na mwaka na pia walikumbana juu ya fadhila za kuangalia vipindi vya MTA.

Wakati wa semina, Rehana Ahmad sahibat aligawa vitabu na majarida ambavyo vilikuwa na maudhui na machapisho mapya ya hivi karibuni kwa ajili ya marejeo.

Aidha washiriki walifanya mtihani ili kupima uelewa walioupata baada ya mafunzo hayo. Washiriki walifurahia hasa kwa kuwa mafunzo hayo yalileta umoja na mshikamano miongoni mwa akina mama kutoka Afrika na msisitizo mkubwa ulitolewa juu ya kumuandikia barua Khalifa wa zama ili kudumisha mapenzi kwa Ukhalifa.

Washiriki hao wa semina hiyo walimshukuru Khalifa wa zama kwa kuwapatia fursa hii ya kihistoria na kumuombea kwa Allah azidi kumpa nguvu na umri mrefu. Mafunzo hayo yalihitimishwa kwa maombi ya kimya.

Baada ya semina hiyo, washiriki hao walipata fursa ya kutembelea kituo cha Ahmadiyya Kitonga ambapo pia waliona ofisi ya Lajna Imaillah Tanzania, Ahmadiyya Sekondari Kitonga na ukumbi wa Jalsa Salana huku wakipokelewa kwa nyimbo na mashairi ya kuvutia.

Wakati washiriki wengine wakirejea katika nchi zao, Mkuu wa kitengo cha Lajna Imaillah Markaz, Rihana Ahmad sahibat, alikwenda mkoani Morogoro ambapo alitembelea hospitali ya Ahmadiyya ya Morogoro, Shule ya Chekechea na ya Msingi, Chuo cha Jamia na MTA Afrika kwenye studio ya Kaluta Amri Abedi.

Ilipofika tarehe 19 septemba muezeshaji wa mafunzo hayo alikwenda Johannesburg nchini Afrika Kusini kwa mafunzo kama hayo. Takribani nchi thelathini zinatarajiwa kunufaika na mpango huu wa kimbingu zikwemo nchi za Ghana na Burkina Fasso.

Ahsante Sana Sheikh Durrani!

Wakati wa Jalsa Salana ya 50 iliyofanyika katika viunga vya Jamaat Kitonga, mwandishi wa maelezo haya alikuwa na majukumu kadhaa yaliyomfanya asipate nafasi ya kuonana na wageni wengi waliofika hasa kwa kuwa hakuweza kutokea jukwaa kuu. Wageni hao waliamua kumtafuta mwandishi huyo kwa sababu walikuwa na shauku ya kumuona. Wageni toka Uganda walifika kwenye banda la huduma ya kwanza walionana nae na kusalimiana kwa bashasha kubwa, wageni toka Kenya pia walipitia na wakaonana kwenye banda la maonyesho kwenye kitengo cha gazeti la Mapenzi Ya Mungu. Tunawashukuru sana wageni wetu wote kwa kuja kwenye Jalsa Salana ya kihistoria.

Mgeni mwingine toka nchi ya Mashariki ya mbali ya Pakistani, ambaye aliwahi kuwa Amir wa Jamaat nchini Tanzania, muhubiri maarufu na msimamizi wa gazeti la Mapenzi Ya Mungu hapa nchini, Sheikh Muzafar Ahmad Durani alimtembelea mwandishi wa maelezo haya katika eneo lake la kutolea huduma. Baada ya kusalimia kwa bashasha Sheikh alisema 'nimekuwa nikimtafuta mudir wa Mapenzi Ya Mungu na nikagundua kuwa umebanwa na kazi nyingi na nimekuja kukusalimia na kukupa zawadi yako toka Rabwah, Pakistani' akamaliza Sheikh Muzafar Ahmad Durani.

Na Akapiga picha ya pamoja na mwandishi wa maelezo haya.

Kwa niaba ya gazeti la Mapenzi Ya Mungu namshukuru sana Maulana Sheikh Muzafar Ahmad Durani. Mwandishi wa maelezo haya hana cha kumlipa Sheikh huyu kwa mapenzi yake kwangu na gazeti la Mapenzi Ya Mungu bali tunamuombea umri mrefu wenye afya tele na aendelee kuitumikia Jumuiya ya Ahmadiyya.

Sheikh Muzafar Ahmad Duran aliondoka siku ya tarehe 13 Septemba kuelekea Nairobi, Kenya.



Ndugu akipewa huduma katika banda la matibabu.



Sheikh Muzafar Ahmad Durani akiwa na wasindikizaji kadhaa waliofika kumuaga uwanja wa ndege wa Julius K Nyerere.

Mfumo wa Ndoa Katika Islam

Imefasiriwa na Abdulkarim Yusuph

MAHUSIANO YA MUME NA MKE KATIKA NDOA

Hapa tunaweza kuona ya kuwa dini tukufu ya Islam imeweza kutuongoza katika maisha ya familia. Majukumu ya mume na mke yameelezwa wazi kabisa kwa ajili ya kila mmoja wao kutambua majukumu yake. Islam inatambua ndoa kama muunganiko wa usawa baina ya watu wawili, ambao wanaweza kupata usaidizi wa Allah katika kushirikiana kwao, uaminifu, kuheshimiana na kuaminiana. Kama wataweza kufuata miongozo iliyowekwa na Allah, wataweza kuwa na ndoa yenye kudumu na yenye kufaulu.

kila mmoja ndani ya ndoa amepangiwa jukumu lake. Allah anasema ndani ya Qur'an tukufu sura ya 20:51

"akasema Mola wetu ni yule aliyekipa kila kitu umbo lake kisha akakiongoza"

mwanaume ameweza kupangiwa kufanya kazi nje ya nyumba akiwa kama mchungaji kwa sababu ya nguvu zake na uwezo wake wa kisaikolojia; vivyo hivyo kwa wanawake ni wazuri kisaikolojia na kihemko katika kulea watoto na wameweza kuwa bora katika kuleta malezi na kuilinda nyumba yao.

kuhakikisha kuwa kunakuwa na ushirikiano safi baina ya mke na mume, mwenza mmoja ameweza kuchaguliwa kuwa ni kiongozi wa familia ambaye ni mume huwa ni kiongozi kwa mke wake, kama inavyosema Qur'an tukufu sura ya 4:35

"wanaume ni walinzi kwa wanawake kwa sababu Allah amewafadhili baadhi yao kuliko wengine; basi wanawake wema ni wale wenye kutii, wanaohifadhi (hata) wasipokuwapo (waume zao) yale aliyohifadhi Allah. Na (wanawake) ambao mnaogopa uasi wao, basi waonyeni na waacheni peke yao katika vitanda, na wapigeni. Na kama wanawatii, basi msiwatafutie njia. Hakika Allah ndiye aliye juu, mkuu."

Hii inaonesha kuwa mwanaume hajapewa haki ya kumkandamiza mkewe katika njia yoyote ile. Inamaanisha ya kuwa anahusika kwa namna yoyote vile kwa ajili ya familia yake na anatakiwa atumie akipatacho kwa ajili ya kuilea familia yake na nyumba yake. Katikia mrejesho, mke anatakiwa kumtii mumewe.

kuheshimiana na kushirikiana ni vitu muhimu katika kujenga mahusiano bora baina ya mume na mke. Allah anasema katika Qur'an tukufu sura ya 2:188

" wao ni nguo kwenu na nyinyi ni nguo kwao..."

Nguo ni kitu kinacholinda dhidi ya baridi, mapambo na kuficha mambo ya ndani. Katika njia nyingine mume na mke wanatakiwa kulindana kwa heshima na maadili, na kumfanya kila mtu kuwa yupo salama



kwa mwenzake. Wanatakiwa wafichiane siri na sio kusema tabia za mwenza wake hadharani.

Mtume mtukufu Muhammad (rehema na amani za Allah ziwe juu yake) alikuwa muwazi sana katika ustawi wa wanawake. Alikuwa akiwashauri wafuasi wake kuwatendea wake zao kwa ukarimu. Yeye alikuwa mfano mwema kwa wake zake. Baadhi ya hadith zasema

1." Mwaminio wa kweli katika suala la imani ni yule ambaye heshima yake ni bora; na mbora kwenu ni yule anayewatendea kwa wema wake zake"

2' "basi mwanaume Muislam hatakiwi kujiburudisha dhidi ya mwanamke Muislam. Kama ameona jambo lisilopendeza dhidi yake, anaweza kutafuta mwingine ambaye anamfaa"

UPANGAJI FAMILIA NA UZAZI WA MPANGO.

Qur'an tukufu imetushauri ya kuwa kunatakiwa kuwepo angalau mpishano wa miaka miwili baina ya uzazi wa kila mtoto ili kuwezesha mwili wa mama kujipanga tena au kurudi katika hali yake. Qur'an tukufu

" Na wanawake waliozaa wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kwa anayetaka kukamilisha kunyonyesha; na ni juu ya baba yake chakula chao na nguo zao kwa sheria; wala nafsi yo yote isikalifishwe ila kwa kadiri ya wasaa wake. Mama asiwekwe taabuni kwa ajili ya mtoto wake, wala baba kwa ajili ya mtoto wake, na juu ya mrithi ni kama hivyo. Na kama wote wawili wakitaka kumwachisha ziwa, kwa kuridhiana na kushauriana, basi si kosa juu yao. Na kama mkitaka kuwapatia watoto wenu mama wa kuwanyonyesha, basi haitakuwa aibu juu yenu kama mkitoa mliyoahidi kwa sheria. Na Mcheni Allah, na jueni kwamba Allah anayaona mnayoyatenda."(sura ya 2:234)

pia Qur'an tukufu inasema

"Na Tumemwusia mwanadamu kwa ajili ya wazazi wake - mama yake amembeba kwa udhaifu juu ya udhaifu, na kumwachisha kunyonya katika miaka miwili - ya kwamba unishukuru Mimi na wazazi wako; marudio (ya mwisho) ni Kwangu"(sura 3:15).

Pia inashauriwa kwa ajili ya uuguzi mzuri wa afya bora kwa mtoto anyonyeshwe ndani ya miaka miwili. Kutoa mimba kunakatazwa sana kama kitendo cha uzazi wa mpango, bali huruhusiwa kama maisha ya mama yapo hatarini.

Uzazi wa mpango unakatazwa kama ukitumika kwa njia ya kuogopa shida za kifedha. Tafadhali kumbuka ya kuwa utumiaji wa uzazi wa mpango kuepuka majukumu ya kulea mtoto kama msingi wa ndoa. Kitu hiki kimekatazwa na dini tukufu ya Islam na si mafundisho ya Islam katika suala la ndoa.

MITALA

Hili ni somo ambalo linaleta na kutafsiriwa kwa maoni potofu dhidi ya Islam kuliko kwengine. Islam inaruhusu mitala. Hii ni kusema kuwa na mke zaidi ya mmoja katika muda mmoja, lakini unatakiwa kujua kuwa jambo hilo halijalazimizhwa. Kwa undani Islam ni dini ambayo imetoa mafundisho haya na kuyatekeleza. Hapo nyuma Islam ilikuwa inakataza ndoa zisizokuwa na hesabu na mitala zisizozuiliwa. Islam imeweka wazi juu ya idadi ya wake wanaoruhusiwa kuolewa ambao mwisho ni wanne, na pia kulielezea zaidi suala hilo. Allah anasema katika Qur'an tukufu.

"...Lakini mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi (oeni) mmoja tu...," (sura ya 4:4)

Kama mwanaume haridhiki na mke mmoja basi ni bora kwake kimaadili na kwa uchumi wake kuongeza wa pili. Kuwa na hawala na kufanya zinaa ni dhambi kubwa sana na husababisha uvunjikaji wa maadili katika jamii.

Mitala huweza kuwa lazima katika sababu fulani, na inatumika inaweza kuwa ya lazima kukiwa na sababu hizo. Mwanaume anaweza kuoa mwanamke mwingine kama mkewe ni mgonjwa wa muda mrefu sana na hawezi kutimiza matakwa ya ndoa; au kama hawezi kushika ujauzito au kupata watoto; au kama katika muda fulani wa vita, kumuoa mjane au yatima kunaweza kuwa lazima kulinda maadili ya jamii. Pia itambulike ya kuwa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya inatambua kuwa Waahmadiyya wanatakiwa kutii sheria zote za nchi husika ambazo wanaishi endapo sheria za nchi hizo hazivunji amri za Allah.

Islam inakataza mwanamke kuwa na mume zaidi ya mmoja. Mwanamke ambaye ameolewa na mwanaume ambaye ni mgonjwa wa muda mrefu, au mume ambaye hazalishi mume anaruhusiwa kutoa talaka, kama wanaona kuwa suala hilo halivumiliki.

TALAKA

Islam inaruhusu talaka, lakini kutokana na hadith, ni jambo mojawapo ambalo la kuchukiza na lisilompendeza Allah. Lakini taratibu za talaka zimeundwa katika muundo wa upatanishi. Chini ya sheria za Kiislam, talaka inatakiwa itolewe mara tatu, katika muda wa mwezi ikipishana kwa kila isemwapo ambapo mwanaume hutakiwa kumwambia mkewe kuwa "wewe si mke wangu". Katika kipindi hiki mwanamke hukaa katika nyumbe (isipokuwa kama atakuwa amefanya zinaa), na upatanishi husisitizwa. Kama talaka ikifikia mwisho, mume anaruhusiwa kumtoa mwanamke huyo kwa njia ya ukarimu na upole". Mwanaume ana jukumu la kuwahudumia watoto wake mpaka wanapofikia umri fulani, na ana jukumu kwa mkewe katika kipindi chote cha eda baada ya talaka.

Baadhi ya sababu ambazo talaka inaruhusiwa ni kama ifuatavyo:

- Zinaa. Lakini kuwe na mashahidi wanne mwenza mshtakiwa anakataa hilo.
- Mume kukataa kuihudumia familia yake.
- Mume kukataa kutoa haki ya ndoa kwa zaidi ya miezi mitatu.
- Unyanyasaji wa kimwili au wa kijinsia kwa mwenza au kwa watoto.
- Kutopatana kwa wenza kufikia kiwango hicho kwamba hawawezi kupatanishwa.

Talaka inaweza kuombwa aidha kwa mume au mke. Kama mume akitaka kuvunja ndoa itaitwa talaka, na hatouliza juu ya urudishio wa zawadi yoyote aliyompatia mkewe. Kama mke akihitaji kuvunja ndoa hiyo itaitwa khula, na itabidi arudishe mahari. Talaka zote hizo kutoka mbili inaruhusiwa au wanaruhusiwa kuoana tena kama wakipatana.

Kwa maelezo na makala zaidi tembelea tovuti ya *www.alislam.org*

Ni Kweli Jalsa Salana ya Miaka 50

Kutoka uk. 1

wanaketi kwa heshima na taadhima. Ulinzi uliimarishwa usiku na mchana. Watoto wanadhibitishwa wasitange tange hovyo huku na huko. Wazee wanapaswa viti vya kukalia sawa na hali yao.

Katibu Mkuu wa Jumuiya, muadham Seif Nakuchima alisoma ujumbe maalum wa maandishi kutoka kwa Khalifa Mtukufu. Ndanimwe mna mwongozo wa kutosha kwa kila mmoja wetu. Tumetakiwa kila mmoja wetu afanye kitu gani. Kwenye ujumbe huo tumetakiwa tuonyeshe sura halisi ya Islam. Tusibeze Tabligh, tusichoke kutoa mali zetu katika njia ya Allah. Tuonyeshe khulka njema wakati wote. Tutangulize dini yetu juu ya mambo mengine. Kwa hili nahisi Mhariri wa mapenzi ya Mungu atatoa kwenye gazeti letu hilo. Iwe hivyo ili hata wale ambao hawakuweza kufika kwenye Jalsa salana hii, wapate angalau kidogo.

Naam, khutuba zilizotolewa na Wabashiri, Masheikh na wataalamu wetu ni chuo tosha cha kujichotea elimu na maarifa mapana ya dini yetu ya Islam. Kwa kweli ninaamini kwa wale wanajumuiuya wapya wamenufaika vya kutosha kabisa. Bali maelezo hayo pia yameongeza nguvu n aari ya uelewa wa mafundisho safi ya Islam kwetu sote. Jazakumullah.

MAAKULI

Ni wakati wa kupata chakula sasa. Ni wakati wa wasiwasi sana khasa kwenye halaiki kama hii. Watu hupata kipapa na mihemko. Lakini hali hiyo kaikutokea asilani. Kuhudumia watu elfu sita si mchezo, ni kazi ngumu kwelikweli. Pamwe na ugumu wote huo, watu walikuwa wanapata chakula bila matatizo yoyote. Chakula kilitosheleza kila wakati wala sikumpata mtu aliyesema yeye hakushiba au amekosa maakuli. Sima, wali mweupe na pilau vilikuwepo.

KWANGU ASTAAJABISHA

Ajabu, lakini ni kweli kweli tupu. Nilifika kwenye maliwato kwa ajili ya kujisaidia. Kule nilimuona Dr. Swaleh Kitabu Pazi Mazongera akiwasaidia wazee kwamba wao wapate fursa ya kwanza kuenda chooni kabla ya mtu mwingine wa marika ya kawaida. Alikuwa anawaeleza watoto na vijana kuwa wao wanaweza kustahimili muda wa saa nzima, lakini kwa mzee hilo kwake halipo. Kwa kuwa mabomba ya chooni yalikuwa hayatoi maji, mwenyewe Dokta alikuwa anakwenda karoni kutwaa maji na kuwapa wazee. Huyu ni mwenye fani ya udaktari. Ni daktari tena basi yupo Muhimbili hospitali. Ilitosha yeye kubaki kuwatibu wana Jalsa Salana watakapokabiliwa na tatizo la afya. Lakini bado aliona hajatimiza wajibu wake! Allah



Amjaze neema na fadhila na apate mafanikio makubwa katika shughuli zake.

SWALA YA TAHAJUD

Ni usiku, umeingia wakati wa usiku. Tulikuwa tunalala mapema ili tusiathiri ibada ya swala ya Tahajud. Kwa kuwa tulikuwa wengi kama nilivyoeleza hapo kabla, watu walikuwa wanajitayarisha tangu saa tisa usiku. Hawa wanakoga na wale wanatawadha kwa kupata udhu. Saa kumi kamili za usiku, swala ya Tahajud ndio ilikuwa inaanza hadi saa kumi na moja Alfajiri ambapo Swala ya Asubuhi ilisaliwa. Baada ya swalatulfajir palikuwapo darasa adhimu. Siku zote tatu za Jalsa Salana hali na mwenendo ulikuwa hivyo.

Kwa kweli zilikuwa siku zenye thamani kubwa sana. Kila mja kuchukuwa alichopta. Sijuwi kama kunja mtu alirejea matupu! Nahisi angalau gao mkononi amerudi nacho. Tafadhali hicho wape ndugu na majirani zako pia nao waneemeke.

REDIO AHMADIYYA

Ustadh Mwalim Abdullah Khamis Mbanga sahib, alipewa nafasi kuzungumzia khabari ya redio yetu. Alisema kwamba Jamaat ya Tanzania imepiga hatua moja mbele. Hivi sasa tuna kituo chetu cha redio kule Mtwara mtaa wa Raha Leo. Redio Ahmadiyya inarusha matangazo yake kwenye masafa ya 99.3 ni ya kwanza katika Afrika Mashariki na kati. Inasikika vizuri sana mikoa ya kusini, kama vile Mtwara, Lindi, Ruvuma hadi Msumbiji. Mwalimu Mbanga aliwataka wajumbe wa Jalsa Salana kuwaambia watu wa kule walikotoka khabri hizi. Aliwataka wanajumuiya wote kusikiliza vipindi vyote vinavyorushwa mutawalia. Redio Ahmadiyya imeanzishwa kwa kusudio la Tabligh. Ni juu yetu kusambaza mafundisho halisi ya Islam.



Kila mwanajumuiya anatakiwa kusikiliza redio hii na pia kupeleka khabari ambazo ndani yake mna ubashiri.

MAKAMBA AWASILI

Tukiwa kwenye kikao cha mwisho jioni, mheshimiwa bwana Januari Makamba, mbunge wa Bumbuli aliwasili ghafla. Hata hivyo, kwa heshima na taadhima, Mbashiri Mkuu na Amir wa Jamaat ya Tanzania Maulana Sheikh tahir M. Chaudhry kabla hajaakhirisha kikao cha Jalsa Salana hii, alimpa nafasi kidogo bwana Makamba kuwasalimu wajumbe.



Mheshimiwa Makamba alisema wazi kuwa yeye si mgeni sana kwenye Jalsa Salana. Alipokuwa Waziri amefika hapa karibu mara mbili au tatu hivi akiwa mgeni rasmi. “Leo mimi si mgeni rasmi. Nimefika hapa kwa sababu zangu binafsi”. Alisema kuwa katika Jamaat Ahmadiyya yeye anao maswahiba wake wawili ambao anashirikiana nao vizuri sana. Hao ni bwana Jamil Idi Mwanga na bwana Abdillah Kombo ambaye walisoma pamoja kule Tanga. “Leo nimekuja hapa jioni hii baada ya kuzungumza na mwenzangu Jamil Mwanga. Yeye aliniambia siwezi kumpata kwa leo kwa sababu yupo kwenye kikao hiki cha Jalsa Salana. Kwa kuwa hapa napafahamu kwa nini nisije? Nimefika nipokeeni” alisema bwana Januari Yusufu Makamba.

Khatimaye akhe makamba aliipongeza Jamaat Ahmadiyya kwa mipamgo yake mizuri ya kukuza elimu ya dini ya Islam kwa watoto. Alinena hivyo baada ya yeye kuwaona mkutanoni hapo baadhi ya watoto waliotoka mikoani na wa hapa mjini wakihudhuria kwenye Jalsa Salana hii. Aliwaona watoto hao wakisikiliza kwa utulivu khutuba mbalimbali zilizokuwa zinahimiza kufuata maadili ya dini yetu ya Islam. “Endeleeni kuwakuza vijana wenu hawa katika utaratibu huu, nao kwa hakika watakuwa wema na wafuasi wazuri walioelimika”, aliishiliza bwana Januari Yusufu Makamba.

Mwishoni, Amir na Mbashiri Mkuu maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alifunga kikao cha Jalsa Salana kwa kuwatakia kheri na salama ndugu wote waliohudhuria. Allah Amfikishe kila mmoja nyumbani kwake salama usalimini na mwakani InshaAllah aweze kuhudhuria tena. Baada ya duwa na maombi ya pamoja, vijana wawili toka Zanzibari, vijana wa Jamia Morogoro na vijana wa Dar es salaam wakiongozwa na mwalim Muhammad Habibu walisoma Kaswida kwa kuwasindikiza na kuwapongeza wajumbe wote. Panapo majaaliwa, Allah Atukutanishe tena mwakani, Amin.

Bustani ya Washairi

BABA YETU MKIETI

Mola wangu Mwenyezi, Jina lako naanzia
Bismillah Azizi, Tungo naiandikia
Kwako kwa Mola kipenzi, pumzi kunipatia
Al watani Mlezi, kilio nimesikia

Al watani Mlezi, kilio nimesikia
Baba yetu mpekuzi, Mola alimjalia
Alimpa na ujuzi, vipaji kumpatia
Kaondoka kama inzi, Akhera ametulia

Kaondoka kama inzi, Akhera ametulia
Hakuwa mwenye ajizi,bashasha alienea
Walimpenda washenzi, waungwana nao pia
Alijazwa na mapenzi, kuhubiri Jumuia

Alijawa na Mapenzi, kuhubiri Jumuia
Mie mazongera pazi, sina la kuongezea
Kweli ifanyike kazi, pengole kulizibia
Tuviandae vizazi, kurithi aloachia

Tuviandae vizazi, kurithi aloachia
Beti tano iwe ngazi, kwenda alipofikia
Shime mkazashangazi, baba yetu alijua
Al watani Mlezi, kilio nimesikia

Pazi Mazongera (kiumbe mzito)
Masanganya-Chamgohi
Kisarawe.

WAPE WATOTO MAADIRI

1. Jukumu ni letu sote, Chukuwa hii habari,
Simama uwe kidete, Watoto lea vizuri,
Madili yote wapate, Wafunzwe vema nidhamu,
Wazazi kuwa makini, Wape watoto maadili.

2. Kuhumiza sala tano, Watubie kwa manani,
Wafundishe sala tano, Wasikutoke kundini,
Na wewe uwe mfano, Wafate yako kanuni,
Wazazi kuwa makini, Wape watoto maadili.

3. Wafate yako kanuni, Kurntukuza manani,
Wasimfate shetani, Kuwapotosha imani,
Vitabu visomwe ndani, Kuwakuza kiimani,
Wazazi kuwa makini, Wape watoto maadili.

4. Tuwalee watoto wema, Waje dini tumikia,
Waitumikie vema, Mola kuwaitikia,
Wazazi simama wima, Madili kuzingatia,
Wazazi kuwa makini, Wape watoto maadili.

5. Tubadilike wazazi, Watoto sipende hadi,
Wape watoto malezi, Wasiwe kiburi hadi,
Funze heshima makuzi, Na simama wima hadi,
Wazazi kuwa makini, Wape watoto maadili.

6. Tuwale kwa umahiri, Wawe na nidhamu nzuri,
Wasiwe wenye viburi, Wawe na nidhamu nzuri
Tuwe mfano mzuri, Watoto siwe jeuri,
Wazazi kuwa makini, Wape watoto maadili.

Madumla Ng'amilo

NAKUMBUKA

Utenzi wa ukiwasili
Kwa bingwa wa Kiswahili
Sheikh mahiri Jamili
Huyo kumhadithia

Na mara ukishafika
Salamu nilokutwika
Mpatie za baraka
Sheikh wetu wa ulua

Masafa hutenga mwili
Na katu sio akili
Hususa hilo muhali
Wampendao Jalia

Wampendao Maliki
Penye furaha na dhiki
Wasiyumbe kwa mikiki
Imara wakabakia

Wampendaye Bashiri
Mjumbe Wake Kahari
Na watengwe na bahari
Huba haiwezi poa

Lugha yetu kasanifu
Hodari na mbunifu
Hadubini tumeshufu
Sana limesaidia

Na bado kwenye luninga
Azidi kutupa mwanga
Hatukosi tukitinga
Elimu kujipatia

Tulifurahi ajabu
Tamu mithili kababu
Shairi lile twaibu
Tanzania tulilia

Hayo machozi ya huba
Yaligusa usuhuba
Pengo lile kuliziba
Ni vigumu imekuwa

Daima tutakumbuka
Kazi iliyofanyika
Atakulipa Rabuka
Mema ulotutendea

Kaditama yadondoka
Machozi yatiririka
Wahadahu Lasharika
Akuhifadhi Jalia

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)

MSILALE

Kwajinale rahamani, wino unanimwagika,
Huu ulimwengu gani, viumbe wanateseka,
Inua macho mbinguni, utandu umetanduka,
Masihi Kateremka, msilale amkeni.

(2) Angalia duniani, kila uchao gharika,
Hamjui ni kwanini, bwana yesu ameshuka,
Mwajemi wa Qadiani, Isa amekwisha fika,
Masihi Kateremka, msilale amkeni.

(3) Sanamu la kipagani, hakika limedondoka,
Mshindo uso kifani, mkubwa umesikika,
Dajjal hoi .shimoni, chini pwaa kaanguka,
Masihi kateremka, msilale amkeni.

(4) Mkitaka duniani, amani yenye hakika,
Fuateni Qur'ani, mwongozo wake rabbuka,
Na Isa mpokeeni, yatawatoka mashaka,
Masihi kateremka, msilale amkeni.

(5) Mashekhe wanazuoni, aya mnazifunika,
Mapadire kanisani, ukweli mnauzika,
Wambieni waumini, yesu wao keshafika,
Masihi kateremka, msilale amkeni.

(6) Yule yesu wazamani, mauti yalimfika,
Mkakamia ishirini, umri aliofika,
Yuko chini kaburini, kashmiri walizika,
Masihi kateremka, msilale amkeni.

(7) Na ondoweni huzuni, ya dunia kuanguka,
Msalaba uvunjeni, baki mungu wa hakika,
Allah tumuabuduni, Asiye na mshirika,
Masihi kateremka, msilale amkeni.

(8) Kumweka isa mbinguni, mbingu zinatetemeka,
Sio ya mungu kanuni, nidhana tu mwaishika,
Haraka sana tubuni, yapungue magharika,
Masihi kateremka, msilale amkeni.

(9) Kifadi tama kituoni, kwenye kiti nainuka,
Kukosa kwetu amru1i, twakadhibisha kufika,
Kwa muokozi wa dini, naye ni dawa hakika
Masihi kateremka, msilale amkeni.

Mwl. Majat Fakim Said Mang'olo =The Big Boss
Ahmadiyya- Pawaga- Magozi- Iringa

MTI

Mti nilioupenda, Leo umeshakauka
Wala sikuupanda, kanitunuku Rabuka
Dahari mi nitakonda, walahi kwakuumbuka
Buriani wangu Mti, Peponi tutakutana

Mti kote ulitanda, bara hadi visiwani
Kocho Kocho ni matunda, uliza a hadi yani
Wengi waliupenda, machoni pia moyoni
Buriani wangu Mti, Peponi tutakutana

Mti kuumwagilia, niliweza mi daima
Leo mejikaukia, sina hata cha kusema
Mwenzenu mi nalia, Mti uwende Salama
Buriani wangu Mti, Peponi tutakutana

Asubuhi na jioni, matunda ulijizalia
Wala sikuona soni, kuchuma na kutumia
Tena nikatia kani, ndugu kuwapelekea
Buriani wangu Mti,Peponi tutakutana

Yalio nifika mazito, ndugu ninawaambia
Lo! Mambo si yakitoto, Mti niliukumbatia
Moyoni mwawaka moto, machoni sitautia
Buriani wangu Mti, Peponi tutakutana

Rajabu mimi nalia, Mola wangu ashapenda
Yanini hii dunia, kumbe sote tutaenda
Kwa Rabi wangu Jalia, Mti uliko kwenda
Buriani wangu Mti, Peponi tutakuta

Mola ilahi Kahari, Mti wangu upokee
Peponi uusitiri, nakivuli uwekee
Mengi yalio ya kheri, uupe usitarehee
Buriani wangu Mti, Peponi tutakutana

Mola wa samawati, mwisho mi nimefikia
Daima wangu Mti, Dua nitauombea
Hadi kwenye sakarati, kifo tapo nijalia
Buriani wangu Mti, Peponi tutakutana

Rajabu Abasi Mkieti AL-WATTANI -_MLEZI
Lusanga Muheza Tanga

NUNGUNUNGU



Ulikuwa ni msimu kali kuwahi kutokea hapo kabla. Wanyama wengi walikuwa kwa sababu ya baridi kali.



Nungunungu waliiona hali hiyo na wakaamua kujiunga na kuwa pamoja ili kupeana joto.

Kwa njia hii nungunungu walijikinga na kujilinda dhidi ya baridi; lakini miiba yao ilikuwa ikiwaumiza wanapokuwa shirika.



Baada ya muda kupita, waliamua kukaa mbali mbali kila mmoja peke yake na wakaanza kufa, kuwa wapweke hadi kuganda.

kwa hiyo iliwabidi wafanye maamuzi magumu...

Aidha wakubali miiba ya kila mwenza au watoweke duniani. Kwa busara, wakakubali kuendelea kuwa shirika tena.

Wakajifunza kuishi na vidonda vidogo vidogo vilivyosababishwa na mahusiano ya karibu na wenza wao ili kupata joto joto linalotoka kwa wengine. Kwa namna hii waliweza kuokoka.



Na shikeni kamba ya Allah nyote, wala msiachane; na kumbukeni neema ya Allah iliyo juu yenu mlipokuwa maadui naye Akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema yake mkawa ndugu; na mlikuwa ukingoni mwa shimo la moto naye Akawaokoeni nalo. Hivyo ndivyo Allah Anavyokubainishieni Aya Zake ili mpate kuongoka. (SURA AALI 'IMRAAN 3:104)

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 29 kwa kuyazungushia na Penseli

W	Y	K	Z	T	D	V	N	Z		B	F	Q		Z	V	M	M	Q	G	X
H	I	N	V	H	G	H	L	U	R	L	V	I	M	L	H	B	T	R	K	X
R	B	S	L	K	H	H	M	Q	X	X	D	T	A	Z	L	P	L	W	I	L
C	U	W	L	M	K	I	T		F	H	W		R	H	I	D	F	K	K	Q
M	X	T	F	A	J	D	D	R	A	T	U	D	K	K	F	R	M	L	O	R
T	H	C	A	A	M	I	A	M	D	B	T	L	A	D	L	K	A	K	K	L
A	R	A	N	N	I	A	P	R	I	K		L	Z	P	V	H	U	A	O	J
D	I	U	N	H	D	D	B	B	U	T	L	M		F	X	I	L	G	T	N
H	P	H	W	D	K	A	A	A	A	B	N	B	D	G	R	L	A	R	O	
K	G	A	L	L	I	T	W	F	D	T	I	X	H	A	J	A	N	T	Z	L
I	T	G	G	A	J	S	A	A	Z		N	N	Y	T	H	F	A	L	I	W
R	I	U	D	R	M	I	I	W	Z	R	T	F	I	B	L	A		Q		K
A	S	P	Q	V	H		G			I		L	J		K	T	L	R	J	J
H	T	A	B	D	L	K	T	T	Q	I		J	P	L	C		F	O	K	P
	I	G	D	T	P	J	A	W	Z	J	I	K	H	L	A	S		M		M
V	G	A	Z	W	M	Q		N	Y	L	H	A	D	U	B	I	N	I		T
H	H	N	M	F	A	H	U	R	U	H	U	B	A	N	I		N	V	N	H
C	F	I	B	L	A	R	T	W	Z	R	P	R	T	A	N	B	I	H	I	
R	A		U	K	U	T	W	A	Q	F	E	E	N		R	T	X	H	J	R
K	R	M	I	K	L	Y	N	L	H	T	M	M	U	A	D	H	A	M		K
B	C	N	T	A	N	Z	I	A		Z	K	F	R	N	C	R	R	K	P	R

Tunatoa pongezi kwa ndugu Saidi Sapi kutoka Kivule kwa kuleta majibu ya Tafuta Maneno ya toleo la mwezi Agosti 2019 ambayo amepatia kwa asilimia 95.

JazakAllah khaira

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Matumizi Sahihi na Bora ya Mitandao

Na Ramadhani Hassani Nauja
Jalsa Salana Tanzania 2019

Muongozo wa Huzoor Aqdas juu ya matumizi ya mitandao ya kijamii
mada niliyopangiwa ni muhimu hususani katika zama hizi za ukuaji wa Teknolojia ya Habari na mawasiliano.

Hakika sote tunaguswa na matumizi ya mitandao ya kijamii katika maisha yetu ya kila siku, hivyo kwa pamoja tunaweza kutafakari na kufikiria juu ya mada hii japo kwa dakika chache.

Mtu anaweza kujiuliza Mitandao ya kijamii ni kitu gani? Je? ina athari yoyote katika maisha yetu?, yapo mahusiano ya kukuwa na kushamili kwake na ujaji wa Masih Aliyeahidiwa na Imamu Mahdi (as) na Je? Ni zipi nasaha za Khalifa wa zama katika jambo hili? haya na maswali mengine mengi ambayo mtu anaweza kujiuliza na kufikiria yanaweza kutupa tafakuri pana na kutufanya tuelewe Zaidi kusudio la mada hii.

Mtandao au Mitandao ya kijamii ni wavuti au huduma ambapo watu huongea au hujumuishwa pamoja. Mitandao ya kijamii inaweza kuunganisha watu wenye shauku au mapenzi ya aina moja kama vile mpira wa miguu, shule, ndondi, vyakula vya aina mbalimbali, filamu, dini, urafiki na kadhalika.

Baadhi ya mitandao ya kijamii ambayo ni maarufu sana duniani ni pamoja na Faceebook 2.3b, YouTube 1.9b, WhatsApp 1.5b, Messenger 1.3b, WeChat 1.1b, Instagram 1b, tweeter 326m, Linkedin 260m, SnapChat 255m na Telegram 200m.

Mitandao ya kijamii inawaleta watu pamoja na kujenga urafiki miongoni mwao na kupeana taarifa. Matumizi zaidi ya mitandao ya kijamii yanaendelea kuvumbuliwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo elimu, biashara, matangazo, siasa, ajira, afya na matibabu, utawala na kadhalika.

Dunia inakadiliwa kuwa na watu bilioni 7.7, kati ya hao watumiaji wa mitandao ya kijamii ni bilioni 3.5, bara la afrika lenye watu bilioni 1.3 kati yao watu milioni 500 wanatumia mitandao ya kijamii wakati nchini Tanzania watu milioni 23 wanatumia mitandao ya kijamii kati ya watu milioni 61.

Takwimu zinaonesha kuwa kila sekunde moja watumiaji wapya 11 hujiunga na kufanya jumla ya watumiaji wapya milioni 100 kuongezeka kila siku katika mitandao ya kijamii, kundi kubwa la wanaojiunga ni rika la vijana.

Watu wengi hujiunga na kutumia mitandao ya kijmii kutokana na faida lukuki za mitandao hiyo, aidha, pamoja na faida hizo ziko hasara pia kutokana na kukosekana kwa usiri na usalama, matumizi ya muda mwingi, picha, video na matangazo mabaya, uhalifu na unyanyasaji wa kimtandao.

Kwa wastani watumiaji wa mitandao ya kijamii hutumia saa 2 na dakika 15 kila siku, ingawa matumizi na muda hutofautiana sawa na jamii na nchi husika, kwa mfano nchi ya Japan hutumia dakika 30 tu kwa siku wakati Ufilipino hutumia saa 4 na dakika 15 katika mitandao ya kijamii kila siku.

Takwimu hizi zinatujumuisha waahmadiyya pia, hivyo yafaa kuchukua tahadhari kubwa, kutafakari kwa kina juu ya matumizi na shughuri tuzifanyazo tuwapo mitandaoni ili kuhakikisha hatuluki mipaka ya Allah na daima tunabaki katika Maamrisho yake wakati wote ili tubaki salama.

Njia pekee ya kubaki salama kwa sasa ni kushikamana na kamba ya mwenyezi mungu yaani Mafundisho ya Islam.

Kuhusina na kufungamana na mafundisho ya Islam, Mwenyezi Mungu anasema;

Na shikeni kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane (3:104)

Mtukufu Mtume Muhammad Mustafa (saw) amenukuliwa akisema:

﴿﴾kitabu cha Allah yaani Qur﴾an ni kamba ya Allah iliyoshushwa toka mbinguni hadi ardhini﴿﴾. (Jarir)

Khalifatul Masih II, Hazrat Mirza Bashir ud Din Mahmood Ahmad (ra) anaeleza kuihusu aya hii ya kwamba:

﴿﴾Vitu vitatu vimetumika kumaanisha kamba ya Mwenyezi Mungu, Vitu hivyo ni Quran tukufu ambayo ni neno la Allah, Mtume wa Allah na Makhalifa wa Allah﴿﴾. (Tafsir Kabir)

Katika zama zetu tumebarikiwa kuwa na Khalifa wa Allah miongoni mwetu, hivyo kushikamana na kamba ya Allah ni kushikamana na Quran, Hadithi na Ukhalifa wa KiAhmadiyya.

Swali linaweza kuzuka, nini maana ya kushikamana na Ukhalifa wa KiAhmadiyya? Ni kujitolea maisha yetu kwa ajili ya Khilafat Ahmadiyya. Ni kutii bila mipaka kila amri njema itolewayo na Khalifa wa zama. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema; "utii hasa ni kuuwa matamanio yetu binafsi yote na kubakiza matamanio ya Mwenyezi Mungu pekee".

Kwa kuzingatia maana hiyo, nitaeleza baadhi ya miongozo ya Khalifatul Masih V atba juu ya matumizi ya mitandao ya kijamii.

Hivyo ikumbukwe tu ya kwamba haya ndiyo matamanio ya Huzoor atba ambayo anapenda wanajumuiyya wote tuishi kulingana nayo kuhusiana na mitandao ya kijamii ili kubaki salama dhidi ya mashambulio ya shetani hususani katika matumizi ya mitandao ya kijamii.

Kuhusiana na facebook Huzoor atba ameeleza mara kadhaa kwamba; "mtandao huo unazo athari hasi Zaidi ya athari chanya na kuwaomba wanaJumuiyya kutumia mtandao huo kwa ajili tu ya shughuli za kijamaat na hususani Tabligh. Ingawa kwa mujibu wa sharia ya Islam haijakatazwa wala kuzuiwa na mtu anayohiyari ya kutumia au kuacha kuutumia mtandao huo". Lakini Huzoor atba anasema; "maendeleo yetu yamefungamana na utii, hivyo yampasa kila Mmoja wetu kuuwa matamanio yake na kutii na kufuata muongozo wa Huzoor atba". Kisa cha Hazrat Aisha.

Kuhusu utumaji na usambazaji wa ujumbe, Huzoor atba anasema katika matumizi ya mitandao ya kijamii tahadhari kubwa inatakiwa kuchukuliwa wakati wa usambazaji na utumaji wa jumbe mbalimbali ili kuepusha makosa kujitokeza na kuchanganywa kwa taarifa au taarifa kutoeleweka vizuri na kutafsiriwa vibaya. Huzoor atba anasema "kabla ya kusambaza au kutuma ujumbe ni lazima ujiridhishe juu ya ukweli na uhakika wa ujumbe huo. Hivyo waahmadiyya wanatakiwa vyanzo vya jumbe na Habari za kweli tu". Kisa cha mwanajumuiyya wa ujerumani, Jalsa.

Kuhusiana na matumizi ya lugha tuwapo mitandaoni Huzoor atba anasema; "tunapaswa kuwa na lugha nzuri na ya staha na tuwe wenye kujiepusha na hasira. Huzoor atba anasema; "anapata taarifa ya kwamba baadhi ya wanajumuiyya wanafikia kuwatolea lugha mbaya viongozi na masheikh kwa sababu tu wako mitandaoni, hii kamwe haikubaliki na si sehemu ya Mafundisho yetu". Kuhusu ibada Huzoor atba anasema; "matumizi mabaya ya Televisheni na mitandao ya kijamii yanamfanya mtu aghafilike juu ya ibada". Mwenyezi Mungu anaserma; "Enyi mlioamini msifuate nyayo za shetani na atakae fuata nyayo za shetani, basi hakika yeye huamrisha mambo ya aibu na maovu, na lau isinge kuwa fadhili za Allah na rehema zake asingalitakasika kamwe miongoni mwenu hata mmoja, lakini Allah humtakasa amtakaye na Allah ni asikiyae ajuaye" (24:22)

Huzoor (atba) anasema; ili kujilinda na shetani kuna ulazima wa kujenga ukuta katika majumba yetu, ambao utazuia mashambulizi ya shetani, kwa kujiepusha kumfanya shetani kuwa rafiki katika maisha yetu, bila shaka kila mwanajumuiyya anatakiwa kujitahidi hasa kupata ulinzi wa Allah dhidi ya Shetani kwa kufanya Istighfari kila wakati. Ulinzi bora hasa dhidi ya shetani ni ulinzi wa Allah tu. Basi katika zama hizi mbaya inatakiwa kufanya sana Istighfar.

Chanzo cha maovu zama hizi ni matumizi mabaya ya Televisheni, mitandao ya kijamii n.k. ukiangali utakuta nyumba nyingi, kuanzia wakubwa mpaka wadogo utaona hawasali sala ya Alfajiri kwa nyakati zake kwa sababu wanachelewa kulala kwa sababu ya kutazama Televisheni au kwa kujishughulisha na mitandao ya kijamii au wakiangalia video/picha ambapo matokeyo yake asubuhi macho yanashindwa kufunguka, kwa hakika watu wa hali kama hii hawajali wala kuzingatia nyakati za sala ya asubuhi kuweza kuamka.

Kuhusu picha, video na program chafu na mbaya mitandaoni Huzoor atba anasema; Mitandao ya kijamii pia ni kitu ambacho ndani yake kuna mambo mbali mbali ya kumfanya mtu ateleze. Kuna kila aina ya mambo machafu yanayoangaliwa ambayo yanaharibu khulka na kwa sababu hiyo nyumba nyingi hazina utulivu, utaona kwamba mke hatimiziwi haki zake wala watoto hawatimiziwi haki zao kwa sababu mwanamume anajishughulisha usiku kuaangalia mambo machafu kupitia Televisheni na mitndao.

Ili kujilinda na shetani, Mtume (saw) alitufundisha dua hii "Ee Allah weka mapenzi yako ndani ya nyoyo zetu, uturekebishe na utuongoze kwenye njia ilionyooka, tutowe kutoka kwenye giza kutupeleka kwenye nuru, tuokowe na maovu ya dhahiri na yaliyofichikana na weka baraka kwenye masikio yetu, macho yetu, kwa wake zetu na watoto wetu na uturehemu kwani wewe ni mwingi wa kupokea toba mwingi wa kurehemu".

Huzoor atba anasema kuhusiana na kujiepusha na upuuzi kwamba; kila mmoja ajichunguze ni kiasi gani anajiepusha na upuuzi na vikao vya kishirikina, wapo wengi sana watakao sema sisi tuna yakini juu ya Mwenyezi Mungu, sisi hatukai kwenye vikakao vya kishirikina, lakin juweni kuwa kikao chochote kile kikiwa cha mitandao ya kijamii, Televisheni

Mahafali ya Ahmadiyya Sekondari Yafana

Kutoka uk. 1

kutojali kitu cha msingi ambacho mwalimu wangu Hamsini Mubiru amekiita "wastwa" katika kitabu cha Ahmadiyya na ukombozi wa Tanzania yaani udajjali wa kuangalia na kuandika historia kwa kutumia jicho moja. Athari yake ni hii sisi vijana wa leo hatutajua kwa usahihi maisha ya baba wa taifa hili.Kuna mifano mingi juu ya wanahistoria kuto nukuu vyema maisha ya mwl nyerere na Taifa kwa ujumla ambayo mwalimu Mubiru ameifafanua vizuri katika vitabu vyake kama Nani aliyebuni jina Tanzania ,Ahmadiyya na ukombozi wa Tanzania,Mwalimu Nyerere na wa Wahmadiyya na Historia ya Ahamadiyya Tanzania,Nami wakati nikipitia magazeti nikakutana na makala inayo husu maisha ya Hayati mpendwa wetu Rashidi Mfaume Kawawa-2.Mwandishi wa makala hayo katika gazeti la UHURU la Januari 2,2018 anadai kuwa Hayati Rashidi Mfaume Kawawa ndio aliyemfikishia Mwl Nyerere wazo la kuanzisha JKT mwaka 1963 baada ya kukutana na kiongozi wa Israel.Ha! nami nashangaa kuona mwandishi wa gazeti nguli kaingia mchomo, kwani wazo hilo la kuanzisha JKT alilitoa Shekh Kaluta Amri Abedi tangia mwaka 1962 katika hali hiyo nikaona tunakazi kubwa ya kubukua katika maktaba zetu.Mapangufu kama haya ndio yalinifanya nijiulize zaidi mwl Nyerere alikua nani na ubingwa huu na umahiri aliyoupata aliupata wapi.Kiherehere hicho kikanifanya nibisho hodi nyumbani kwa mwalimu Hamsini Mubiru nikamkuta nilipo mueleza haja yangu kuwa ninataka kumjua baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alinijibu jibu moja kuwa tujifunze maisha ya mwl Nyerere akiwa Tabora.Hapo ndipo niliona kazi yangu imekuwanyepesi kwangu kwani nimepata pakuanzia. Wala siku shangaaa tena palenilipo muona Raisi wangu mpendwa wa Jamhuri ya Tanzania Mh John P. Magufuli aliposema mradi mkubwa wa uzalishaji wa umeme katika bwawa la mto Rufiji utaitwa kwajina la Mwl Nyerere,bali hata kuzubaa sehemu mbalimbali kupewa jina la Mwl Nyerere kama vile uwanja wa ndege wa kimataifa wa Dar es salaam,Barabara ya Mwl Nyerere nk.Kwa hakika hii yote ni nijitihada kubwa ya kuungwa mkono.Lengo la yote haya ni kutaka kuona thamani ya Mwl Nyerere inabaki na kurithishwa kwa vizazi hadi vizazi.Sasa sifa hizo zinazo miminwa na wasomi kwa mwl Nyerere kuwa alikua kiongozi na sio mtawala,alikuwa mtu aliyependa ushauri nasio mabavu, alikua mtu aliyekubali kujifunza na kusoma sana vitabu hadi mwisho wa maisha yake kama anavyo eleza mwenyewe katika barua yake aliyo mjibu shekh Mubaraka Ahmadi 21 june 1985,yote hayo na sifa nyinginezo zote tunaweza kufaidika nazo kama kweli tutafata na kujifunza maisha ya mwl akiwa Tabora kama alivyo nijibu mwl wangu Hamsini Mubiru.Niyapi hayo maisha ya mwl Nyerere akiwa Tabora?. Bila shaka hili ndilo swali linaweza kuzuka kwa msomaji wa makala hii, jibu lake ni hili kuwa mapinduzi ya kifikra na mtizamo aliyo yapata Mwl Julias Nyerere akiwa Tabora Boys (ya wavulana) kutoka kwa Maulana shekh Mubaraka Ahmadi ndiyo yalio mtengeneza Mwl Nyerere kuwa mtu mahiri na mwenye mitizamo chanya hata baadae katika harakati za kisiasa akadihirisha kwa umahiri wake huo wa hali ya juu ambao umeendelea kukaririrwa na waandishi wengi pamoja na wasomi katika majaridi na mihadhara ya kumbukizi yake.Wapo wanaoweza kuibeza hoja hii lakini nivyema wakafahamu hata iweje mbegu iliyo bora ikipandwa katika changarawe kwa hakika haitaota kamwe.Kama Mwl Nyerere aliweza kumea na kunawiri katika ulingo wa siasa basi Maulna Shekh Mubaraka Ahmadi alifanya kazi kubwa ya kumwagilia mbengu hiyo kila mara na kuisimamia ili kumea vyema katika udongo mzuri.Ni lazima tukiri kuwa mti hujulikana kwa matunda yake. Tunda moja wapo la shekh Mubaraka Ahmadi ni Mwl Julias Nyerere.Shekh Mubarak alimuandaa Mwl Nyerere kuwa tayari kujitolea katika kila hali,alimfanya kuwa mpenzi mzuri wakusoma vitabu kwani Mwl aliweza kusoma vitabu vya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya na vinginevyo vilivyo mjenga kuwa mpigania uhuru mahiri na jasiri.Kwani kama vile alivyosema Rais mstaafu Jakaya M.Kikwete katika kongamano moja la kumbukuzi ya Mwl Nyerere kuwa Mwl Nyerere aliweza kuacha kazi ya uwalimu ya mashahara mkubwa na kujiunga na harakati za uhuru kwa kazi isiyo na mshahara tena bila kujua kama baadae angefanikiwa kushika hatamu katika nchi, bila shaka hayo nimaandalizi yaliofanya na shekh Mubarak Ahmad kwa Mwl Nyerere kuwa njia bora ya siri ya jambo lolote la mafanikio liko katika kujitolea kwani hii ndio sifa kubwa ya waahmadiyya.Hivi leo ni lazima tujue kweli kama tunataka kumuenzi kweli mwl nyerere ni lazima tuige mfano wa kujifunza njia aliyo ipitia kuipita akiwa Tabora pamoja na kusoma vitabu vya Jumuiya ya Ahmadiyya ndivyo vitakavyo leta mapinduzi makubwa katika Taifa hili na kutengeneza mustakabali wa nchi hii.Bila shaka kwa njia hii tutakuwa tumemuenzi mwl Nyerere kwa vitendo na sio kwa maneno.

Mahafali ya Ahmadiyya Sekondari Yafana

Kutoka uk. 1

na uboreshaji wa mabweni ya wavulana. Mabweni haya yameongeza tija katika ulinzi na usalama wa wanafunzi na kutoa mazingira salama ya kujifunzia, Alisema meneja.

Aliendelea kueleza kuwa, ujenzi wa Jiko na stoo zake, bwalo la chakula na sambamba na uboreshaji wa huduma ya chakula na kuhakikisha afya na usalama wa wanafunzi wote inapatikana kwa muda wote.

Mkakati wa kuongeza idadi ya walimu kutoka 13 hadi 24 ulihakikisha ubora wa Elimu unapatikana, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa wanafunzi, na kuongeza jitihada ya wanafunzi kujisomea, mitihani na masahihisho. Vipindi vingi vya ziada vilibuniwa, mashindano ya Shule na Shule kitaaluma na michezo iliongezeka na leo tu tunao wakuu wa Shule watatu kuja kutuunga mkono katika Mahafali yetu haya, ilisema taarifa yake.

Aidha viwanja vya michezo vya mpira ya miguu na mpira wa mikono nazo vikaongeza changamoto kwenye kujenga afya za wanafunzi, Mashindano kadhaa yalifanyika na kutekeleza dhana ya michezo kwa afya na kuboresha afya ya wanafunzi kisaikolojia.

Kupatikana kwa huduma ya umeme wa uhakika, Huduma ya Zimamoto, Mazingira, Uhakika wa maji na Huduma ya afya na tulizingatia vya kutosha matibabu ya wanafunzi ili kuhakikisha siku zote wanafunzi wanabaki katika afya zao na ili waweze kusoma salama na afya nzuri.

Haya hivyo, tuliamini na tunaendelea kuamini kuwa nidhamu haitokani na Elimu ila nidhamu ya kweli hutokana mtu kuwa hofu na Allah wake. Hivyo tulihamasisha kila mwenye Dini yake kusali na kwa wale Waislamu tukawajengea msikiti ili kuhakikisha hili linatimizwa. Wanafunzi wakristo walipewa ruhusa kwenda kuabudu kwenye siku zao za Ibada. Tukaanzisha vipindi maalumu vya kufunza Dini hasa ya Kiislamu kwa Waislamu na leo hii watazawadiwa kushuhudia maendeleo yao. Hii ikapelekea Shule yetu isikumbwe na matukio ya nidhamu na hakuna aliyesimamishwa au kukutwa na kesi ya kinidhamu. Alisema Mussa Mgeleka sahib.

Alimueleza Amir Jamaat kuwa jitihada kubwa zako za kuwa bega kwa bega na Shule, wazazi kuisaidia Shule, Walimu na watumishi wote wa Shule kwa pamoja wamewezesha kuona matunda haya ya leo. Na wanafunzi hawa ni matokeo ya Jitihada zenu nyote. Ni matarajio yetu wanafunzi hawa kufanya vizuri zaidi kulinganisha na miaka ya nyuma. Tunakijana aliyepata daraja la kwanza kwa alama 7, akiwa form two anamaliza leo naye ndiye amepata tena daraja la kwanza kwa alama 7 kwenye mtihani wa Shule binafsi na amekuwa wa kwanza pia katika Shule hizo. Aliendelea meneja kueleza.



Amir Jamaat Sheikh Tahir Mahmood Chaundry, akiwa na wahitimu wa kidato cha nne kwa mwaka 2019 katika siku ya mahafali yao Kitonga.

Baada ya kupata maelezo hayo Amir Jamaat, Sheikh Tahir Mahmood Chaundry aliwatunuku vyeti wahitimu na Walimu wao, kuonyesha shukrani kwa Jitihada zao. Pia vilitolewa vyeti vya kumaliza shule, Zawadi ya Mwanafunzi bora, Mwanafunzi bora wa Kike, Nidhamu, Usafi, zawadi kwa Washindi wa Elimu ya Dini na Walimu kutoka Idara ya Kiswahili, Idara ya Taaluma, na Maarifa ya Islam nao walipatiwa zawadi kwa jitihada zao.

Mheshimiwa Amir Sahib, katika mahafali hayo alisema kuwa leo ni siku ya furaha na katika kanuni ya furaha, furaha huwa haikamiliki bila kumshirikisha mwenzio. Amepongeza kazi nzuri inayofanya na uongozi wa shule na mafanikio hayo ni ya kujivunia sana. Kuwaita wazazi na wanafunzi wote kusherekea ni jambo jema sana na pia aliwaomba wanafunzi wote na wanafunzi wakafikishe furaha hizi kwa wazazi wao na walezi wao na ndugu na Jamaa. Fadhili hizi tulizojaliwa na Allah na wanafunzi kuwa sehemu ya kuneemeka basi wazitumie kuwahamasisha wenzao na ndugu na Jamaa kuleta watoto wao kwenye Ahmadiyya Secondary. Tunapokea wanafunzi wa Kidato cha kwanza, na wanaohamia pia kwa sababu mbalimbali.

Kwa niaba ya Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Amir Sahib aliwaomba wahitimu wa Mahafali haya kufikisha Salamu zetu za Shule kwa Wazazi na Walezi wao, ndugu na Jamaa wote na jukumu letu la mafunzo na malezi tumelihitimisha na tunaombea kwa Allah wakafanye mitihani yao kwa salama na Ufaulu na wakawe vijana bora na wenye kutumainiwa kwa Taifa letu na kumtumikia Allah.

Matumizi Sahihi na Bora ya Mitandao

Kutoka uk. 8

au kazi yoyote inayokughafilisha kusali sala basi hicho ni kikao cha kishirikina.

Kuhusu umuhimu wa kuinuwa kiwango cha haya (aibu), Huzoor (atba) anasema; "Uvumbuzi mpya wa mambo ya kidunia kama vile Televisheni, mitandao ya kijamii n.k zimebadilisha kabisa historia ya mazingira ya haya (aibu), baada ya maovu kuwa wazi sana, basi watu wanasema haya sio maovu. Hali ya aibu ya mwanajumuiyya haitakiwi kuwa kama ya yule anaye tizama televisheni na mitandao, kwani hii siyo haya bali ni kutekwa na matamanio. Hata badhi ya nyumba za wanajumuiyya utakuta hakuna stara wala haya eti kwa sababu inadaiwa kuwa ni Maendeleo na usasa au kwenda na wakati. Kama wanajumuya hawazitakasa nyumba zao dhidi ya maovu haya, basi ile ahadi ya utii waliyo shika kwa Imam wa zama imevunjika na imani zao zimeharibika. Mtume (saw) anasema "Haya ni sehemu ya imani".

Huzoor atba anaendelea kusema "basi kila mwanajumuya hasa vijana inatakiwa wazingatie kuhusu maovu ya siku hizi yanayo sababishwa na vyombo vya kisasa vya habari, wasijihusishe nayo lasivyo imani zao zitaharibika. Kutokana na athari ya maovu hayo baadhi ya watu wanao jihusisha nayo wanaruka mipaka yote ya Mwenyezi Mungu mpaka wanafikia hatua ya adhabu ya kutolewa nje ya Jamaat. Hivyo kila mmoja azingatie kuwa siku zote kila kazi aifanye kwa kupata radhi ya Mwenyezi Mungu".

Huzoor Anwar (atba) anatuongoza kulinda kizazi chetu kutokana na maovu mitandao ya kijamii, Huzoor atba anasema; muda mwingine watoto pia wanavunja hukumu za Mwenyezi Mungu, hii pia ni aina fulani ya shirki. Kukataa hukumu ya Mwenyezi Mungu iliyowazi na kufuata matakwa ya watoto nayo ni aina fulani ya shiriki iliyo fichikana. Vitu hivi vya kidunia muda mwingine vinasahaulisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu, watu wengi wamejitenga mbali na Ahmadiyya kwa sababu ya watoto wao. Siku hizi watoto wanaoshi hapa wana maradhi haya kuwa, wanakuwa wanawaomba wazazi wao "tununulie simu" mtoto mdogo mwenye umri wa miaka 10 anataka simu, eti lazima na sisi tuwe na simu! Kwani ninyi mnabiashara gani au kazi gani? inayokusababisha kila dakika kupiga simu ilikujua inaendeleaje? Ukiwauliza mnataka simu za kazi gani wanasema "tunataka kuwapigia wazazi wetu", basi kama wazazi hawaoni umuhimu wa kuwapatia simu basi nanyi hamlazimiki kuomba kupewa. Kwani simu inasababisha mazungumzo mabaya, simu inamsababishia mtoto kuwa na tabia mbaya, kwenye simu kunakuwa na program kama vile katuni hata baadhi ya program mbaya wanaangalia lakini inatakiwa watoto wakatazwe kuangalia program kama hizo. Ni kazi ya wazazi kuwachunguza watoto wao juu ya matumizi ya simu. Sio vizuri kila muda mtoto kushika simu. Na wale kina mama wasiojua kutumia simu au kompyuta wajifunze ili waweze kuwachunguza watoto wao.

Huzoor (atba) anaendelea kusema kwamba kwenye Televisheni pia kuna program chafu nyingi sana, kwahio wazazi wanatakiwa wazi zuie zile chanel zinazo onyesha program chafu na kusababisha athari mbaya kwa watoto, ni jukumu la wazazi kuhakikisha kuwa chanel mbaya zote wanazizuia na kuhakikisha mtoto anaangalia chanel safi na nzuri tu, mtoto mwenye miaka 12 anakuwa mwenye kujitambua kwa hiyo ni wajibu wake pia kujiepusha na vitu hivyo.

Huzoor atba anasema basi dumuni kuomba dua hii; "Ee Mola wetu, utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho na utujaliye kuwa viongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu"(25:75)

Ili Kujiepusha na madhambi ya dhahiri na siri Huzoor Anwar atba anasema kwamba; "Mwenyezi Mungu anasema usiyakaribie maovu. Yaani mambo yote yanayo vutia kwenye uovu usiyakaribie kwa kujiepusha. Kama vile zama hizi kuna mitandao ambayo ndani yake kuna upuuzi mwingi, ndani ya website, Televisheni kuna filamu chafu, kuna vipeperushi vichafu ambavyo vinazungumzia habari za pornography na n.k., haya yote ni maovu yasikaribiwe kabisa, kwani mtakuwa watu waovu. Maovu haya yatawawekwni mbali na Mwenyezi Mungu, pia yatawasababisha mvunje hukumu za Mwenyezi Mungu. Kila mmoja azingazie hukumu hii ya Mwenyezi Mungu kwamba hakuna kukaribia maovu la sivyo shetani atawakamata tena.

Mitandao ya kijamii na hususani MTA ni nyenzo muhimu katika kufungamana na Ukhalifa wa Kiahmadiyya, Huzoor (atba) alisema; "katika zama hizi Jumuiyya ndio inatumia ipasavyo Televisheni, mimi nimekuwa nikiwahimiza wanajumjuiyya hata katika kipindi cha Jalsa kutizama MTA wengi wao wameathirika, baadhi yao wananiandikia kwamba mimi nilikuwa siangalii MTA hapo kabla, lakini baada ya wewe kutuhimiza tumeanza kuangalia na tunasikitika na kujuta kwamba kwanini hapo kabla tulikuwa hatuangalii? na kwanini hatukufungamana nayo (MTA)?◎.

Wengine wanasema, baada ya kutazama MTA kwa siku kumi tu tumepata mabadiliko makubwa ya kiroho na elimu yetu imeongezeka maradufu, sasa hivi ndio tumeifahamu vya kutosha Jumuiyya ya Ahamdiyya.

Basi nawakumbusha tena juu ya MTA kwamba jitahidini kufaidika na neema hii ambayo Allah ametupatia kwa ajili ya kujiongezea elimu na kupata malezi ya kiroho ili kizazi chetu kidumu kushikimana na Ukhalifa. Sote tunatakiwa tujitahidi kadri ya uwezo wetu kushikamana na MTA. Sambamba na hotuba zangu siku hizi kuna program nyingi ambazo zinarushwa mubashara ambazo tunaweza kunufaika na mambo ya dini na kiroho na kuongeza viwango vyetu vya elimu.

Huzoor atba anaendelea kusema; "Wasio kuwa wanajumuiyya wananufaika nayo na wanapata kujua ukweli wa Ahmadiyya sambamba na hayo wanapata kujua kuhusiana na Tauhidi (umoja wa Mwenyezi Mungu) na ukweli wa Islamu. Na barakara nyingine ni hii kwamba MTA ndio chanzo cha kupata Baraka zinazo ambambatana na Khilafat Ahmadiyya".

Kuhusiana na mahubiri, Huzoor (atba) anasema; "kitengo cha Tabligh cha Lajina wanatakiwa watengeneze timu ya mahubiri ambayo itawahusisha wanawake na weasichana tu, lazima mfahamu kuwa mahubiri kupitia mitandao ya kijamii ya lajna yawe kwa ajili ya Lajna tu. Hivyo wale wanao fanya mahubiri kupitia mitandao ya kijamii wawe wanawake kwa wanawake tu na wanaume kwa wanaume tu. Kwani muda mwingine hutokea maovu, eti kwa masingizio kuwa sisi tunafanya mahubiri. Hali hii huleta matokeo mabaya kwa mtoto wa kike wa ki Ahmadiyya".

Kuhusiananamahubirimitandaoni Huzoor (atba) anaendelea kusema; "Review of Religions ni jarida lililoanzishwa na Hadhrat Ahmad (as) mwaka 1902. Mpaka sasa miaka 114 imeshapita, kwa fadhili za Allah katika zama hizi platform mbalimbali zimekuja. Kwa msaada wa Allah jarida la Review of Religions linapatikana kwa sasa kupitia mitandao ya kijamii pamoja na YouTube. Ujumbe wa Islam unaenea kupitia jarida hili. Kupitia platform hizi mamilioni ya watu wanapata ujume wa Islam". ROR kwa hapa kwetu.

Pia Huzoor (atba) anasema kuhusu kueneza ujumbe wa Islam kupitia mtandao wetu wa alislam.org kama; "kwenye mtandao wetu wa alislam.org kwa fadhili za Allah kuna kitu kipya kimeongezwa sasa hivi wametengeneza (search engine) ambayo kwa mfano ukitaka kutafuta neno Allah au Yesu Masih (as) au Muhammad (saw) basi unaandika kwenye (Search Engine) inakuletea mara moja maandiko ya Seyyidna Ahmad (as) pamoja na nukuu zake kutoka kwenye vitabu vya Seyyidna Ahmad (as) vilivyo kusanywa kwenye Rohan Khazain".

Khalifa Mtukufu atba akizungumza kuhusu Baraka za MTA, anasema; "katika zama ambamo tumo, sio nchi moja tu hapana bali ni hali ya duniani kote, kwamba vyombo vya habari vimetufanya tuwe karibu kama kijiji, kwa bahati mbaya badala ya vyombo vya habari kutuleta karibu na wema inatuleta karibu na shetani. Basi katika hali hii kwa mwanajumuiya anatakiwa ajichunguze hali yake. Kwani Allah ametupatia MTA na mitandao kwa ajili ya kuji imarisha kiroho na kujiongezea elimu ya Jumuiyya".

Huzoor (atba) anaendelea kusema; "nimekuwa nikiwahimiza mara kwa mara wanajumuiya kwamba program zinazooneshwa kwenye MTA inawapasa waziangalie. Wazazi pia wazingatie hilo na wawahimize watoto wao kushikamana na MTA. Kwani hii ni chakula cha kiroho ambacho ndio chanzo cha kukufanya ubaki hai kiroho. Kutokana na MTA elimu yako itaongezeka, utapata maendeleo ya kiroho na utakuwa na uhusiano madhubuti na nidhamu ya Ukhalifa na utakuwa umeokoka na sumu ya vitu vya kidunia".

Hivyo ndugu zanguni ni hitimishe kwa kuwaomba ya kwamba daima tushike nasaha za Khalifa wetu mpendwa, tudumu kushikamana na MTA na mtandao wetu wa alislam.org, kufanya istighfar na kuomba maombi yote ambayo Huzoor atba ametufundisha, kumswalia mtume (saw), kufuata maamrisho yote ya Quran tukufu na Hadithi za mtukufu Mtume Muhammad (saw) ili kujinusuru kutokana na mashambulizi ya shetani kupitia mitandao ya kijami.

Ninamuomba Allah atuwezeshe sote kutekeleza nasaha hizi za Khaliful Masih wa V atba. Amin

Ujenzi wa Misikiti na Majukumu Yetu

Inatoka uk 12

bidii cha mtu katika sala kinatakiwa kiwe kama hali hii ya kuungua. Wakati mtu akifikia hali hii kama ya mtu anayekaribia kufariki, hiyo ndio Sala ya kweli. Hivyo, huu ndio uhalisia wa Sala ambao sisi sote tunapaswa kujaribu kuufikia; Mwenyezi Mungu Aturuzuku uwezo wa kufanya hivyo.

Aidha akielezea hili zaidi, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kuwa watu wajinga wanahoji kwa nini Mungu Mwenye Enzi ana haja ya maombi yetu "Masihi (as) anasema:" Enyi watu wajinga! Mwenyezi Mungu si mhitaji wa kitu chochote, bali kwa hakika ni wewe ambaye unayahitaji maombi ili kwamba Mwenyezi Mungu Akugeukie upande wako. Kila kazi isiyokamilika inaweza kukamilika ikiwa Mwenyezi Mungu atakuwa pamoja nawe. Maombi yanaweza kuondoa maelfu ya madhambi na kuwa chanzo cha kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hata wakati wa kusubiria Sala katika msikiti, Malaika wa Mwenyezi Mungu huomba kwa ajili ya mtu aliyehudhuria msikitini kwa ajili ya Sala. Hivyo, tunapaswa kuonyesha kujali sana ili kutimiza haki za ibada ya Mungu Mwema kiasi hicho na kuhudhuria msikitini kwa sala zote tano za kila siku. Wakati akielezea ukweli kwamba lengo la dini ni kustawisha umoja na kujenga jamii moja; Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema: "Madhumuni ya dini pia ni haya kwamba jamii ya wanadamu iweze kuunganishwa mfano wa punje za vidani vya Tasbeeh (Rozari) kupitia mkufu mmoja. Sala za Jamaa pia zipo kwa madhumuni hayo ya kuunganisha ili kwamba waabuduji wote wahesabiwe kama kitu kimoja. Hii ni kukuza umoja kila siku, kisha kila Ijumaa mkusanyiko mkubwa zaidi unakusanyika kukuza umoja na hatimaye Hajj ni kukuza umoja katika dunia yote. "



anasema: Basi enyi watu wote mnaojihesabu katika jamaa yangu! Hamtahesabiwa mbinguni katika jamaa yangu mpaka mtembee katika nyayo za utawa kweli kweli. Basi simamisheni sala zenu tano kwa unyenyekevu na upole wa moyo kama ni wenye kumuona Mwenyezi Mungu Mtukufu. ... Kwa hiyo jihadharini ili msiteleze. Ardhi haiwezi kuwadhuruni hata kidogo ikiwa mmefungamana sana na mbingu. Wakati wowote ikikupateni dhara basi itakuwa inatokana na mikono yenu na wala sio mikono ya adui yenu. Na kama ikiondolewa heshima yenu yote ya duniani, Mungu Atawapeni heshima ya milele mbinguni, basi kwa hiyo msimwache kabisa.

Allah Mwenye Enzi Atuwezeshe kuelewa maneno haya yaliyotoka moyoni hasa mwa Masihi Aliyeahidiwa (as) na kutuwezesha kuongezeka kwa imani zetu. Yeye Atuwezeshe kutimiza haki za kuabadu na kutuwezesha kuzalisha mahusiano imara na Mwenyezi Mungu, na Atuwezeshe kuweza kuujaza msikiti huu muda wote.

Kisha Hazrat Khalifatul Masihi (V) atba akatao baadhi ya maelezo kuhusu msikiti huu. Uwezo rasmi wa msikiti huu ni kwa ajili ya watu 250 kusali, ambao halmashauri wa mahesabu yake, kuna nafasi ya maegesho ya gari kwa ajili ya magari 50, ofisi moja kwa ajili ya Jumuiya, ofisi ya Lajna, maktaba kwa wanaume na wanawake na kuna huduma ya vyoo vya kutosha. Ukumbi mkubwa wa maegesho umeezekwa na kama wakati wowote kunatokea dharura, kuna nafasi kwa zaidi ya watu 125 kusalia hapo. Msikiti huu uko takriban kilomita 15 kutoka Strasbourg. Eneo lililojengwa kwa ajili ya msikiti na kumbi zingine ni mita za mraba 303. Pia kuna nyumba ya Mbashiri, pamoja na vyumba vinne vya kulala kwenye nyumba ya wageni. Ruhusa haikutolewa kwa ajili ya ujenzi wa mnara, hata hivyo, ruhusa ilitolewa kwa ajili ya kujengwa kuba, ambayo ipo kwenye kimo cha mita 8 na ipo upande wa kulia wa msikiti.

Mwenyezi Mungu, Aubariki msikiti huu kwa kila jiha na pia Aubariki sana uzao na Azibariki mali za wale Khuddam ambao wamejitolea ili kujenga msikiti huu. Mwenyezi Mungu Ajaalie kujitolea kwao kusiishie katika sadaka ya kifedha peke yake, bali pia Mwenyezi Mungu Awawezeshe kuelewa umuhimu wa kuijaza misikiti. Mungu Mwenye Enzi, Ainue kiwango cha ibada cha Khuddam na pia Ainue kiwango cha ibada cha Wanajumuiya wengine. Amin.

Masahihisho

Katika toleo maalum la Mapenzi Ya Mungu kwa ajili ya Jalsa Salana ya 50, tulieleza kuwa Waziri Mkuu mstaafu, Mheshimiwa Frederick T Sumaye alihudhuria Jalsa Salana ya mwaka 2004 kwa mara ya kwanza iliyofanyika katika viunga vya Saba Saba. Hii siyo sahihi.

Mheshimiwa Sumaye alihudhuria Jalsa Salana kwa mara ya kwanza kabisa katika Jalsa Salana ya mwaka 2002 iliyofanyika katika viunga vya Mnazi mmoja Amir Sahib akiwa Sheikh Muzafar Ahmad Durani.

Tunaomba radhi kwa mkanganyiko huo na tunawashukuru wasomaji wetu kwa kutukumbusha historia hiyo.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

MUHH.-SAF. 1439 AH | NOVEMBA 1-15 2019 | TABOOK 1398 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

.Imesimuliwa na Hadhrat Jabir r.a. kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Mfano wa sala tano ni kama mfano wa mto uliojaa maji unaopitia mlangoni pa mmoja wenu, naye anaoga humo kila siku mara tano. (*Muslim*)

Ujenzi wa Misikiti na Majukumu Yetu



Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba katika msikiti uliofunguliwa hivi karibuni huko Strasbourg nchini Ufaransa.

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 11/10/2019 aliyoitoa Strasbourg nchini Ufarasa katika uzinduzi wa msikiti; baada ya Tashahhud, Taawwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Momeneen, Mirza Masroor Ahmad atba alisoma aya za 18 ya Surah At-Taubah pamoja na tafsiri yake kama ifuatavyo: "Anayestawisha misikiti ya Allah ni yeye tu amuaminiye Allah na siku ya mwisho na kusimamisha sala na kutoa zaka na hamuogopi yeyote ila Allah, basi hao huenda wakawa miongoni mwa walioongozwa."

Kisha Khalifa Mtukufu atba akasema:

Baada ya kipindi cha muda mrefu, Mwenyezi Mungu, Mwenye Enzi Ameiwezesha Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Ufaransa kujenga msikiti mwingine katika nchi hii. Katika mji wa Strasburg, asilimia 75% ya Waahmadiya sio wa asili ya Pakistani na kwa baraka za Allah, wanajamaat hawa ni wenye imani ya dhati sana na waaminifu. Sasa, Waahmadiya wanaoishi hapa wanaweza kukuza uhusiano wenye nguvu zaidi na Jumuiya kuliko hapo kabla. Allah, Mwenye Enzi Awawezeshe kufanya hivyo.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameeleza sifa za watu ambao hujenga na kuijaza misikiti kwamba wana imani thabiti juu ya nguvu kubwa ya Mwenyezi Mungu, ambayo Hashirikiani na mwingine yeyote. Wao wanaamini katika siku ya hukumu. Wanayo imani juu ya maisha ya Akhera ambayo inawafanya kuwa makini juu ya kufikia mwisho mwema. Watu hawa husimamisha sala kwa jamaa, hujitolea kifedha na hujitahidi kusonga mbele kueneza mafundisho ya Kiislamu na kutimiza haki za wengine. Matendo haya yote mazuri huwafanya kuwa makini zaidi na kufahamu utukufu na nguvu ya Mwenyezi Mungu na wanajitahidi kupata radhi Yake. Watu hawa ndio watu walioongoka mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Waahmadiyya wapya waliojiunga na wale ambao ni wa kuzaliwa ndani ya Jamaat wote wanapaswa kuzingatia - na kwa hakika, Waahmadiya wakongwe, hasa wale ambao wanatokea Pakistan, wanao wajibu mkubwa zaidi wa kukumbuka kwamba - kwa hakika wanatakiwa kuwa mfano mzuri kwa Waahmadiyya wapya. Waahmadiya wote ni lazima kwanza kabisa kutathmini Sala zao na kuona kuwa, ni ndio au hapana, kwamba wao ni wenye kuzingatia Sala zao tano za kila siku na kuzisali kwa kudumu tena kwa jamaa. Inahitajika juhudi na kujitolea kikweli kwa mtu kuweza kusali vizuri ipasavyo pamoja na kubaki mwenye mazingatio katika Sala na kujikinga na wasiwasi na mawazo mengine. Sala ya kweli humfanya mtu kuzingatia majukumu yake kwa viumbe wenzake na kuwasaidia katika njia ya Taqwa (uchaji Mungu). Falsafa nzima ya Uislamu ni kumwezesha mtu binafsi kutumia vipaji vyake vyote kwa njia ya haki na ucha Mungu. Watu, ambao wanaelewa na kujichunga kwa namna hii, hao kweli ndio walioongoka na hatimae ndio wenye kushinda.

Akielezea hali ya Sala ya kweli, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema, "Sala kwa hakika haimaanishi tu kufanya matendo fulani ya kimwili na kutenda tu kama mazoezi au kama jambo la kimila. Katika Sala ni mahali ambapo moyo wa mtu unahisi roho kuyeyuka na katika hali iliyokithiri hofu unaporomoka mbele ya kizingiti cha Mwenyezi Mungu. Hiyo ndio Sala iliyojaa baraka. Kama mtu atashikilia kwa kudumu kwenye hali hiyo basi kwa haraka muda utafika, ikiwa mchana au usiku, ambapo mtu atashuhudia kwamba mwanga wa kiroho umeushukia moyo wake na asili ya ukachu wa nafse Amara [nafsi yenye kuamrisha maovu] imepungua." Kwa maneno mengine, ni Mwenyezi Mungu Peke Yake, Ambaye Anaweza kumlinda mtu kutokana na ugonjwa huo, hivyo mtu ni lazima kwa kudumu aombe kupata baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Akitufafanulia kuhusu umuhimu wa Sala, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba: Sala ndio kiini cha maombi na wakati wa kusali, mtu lazima daima akumbuke kwamba anapaswa kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa heshima kubwa na adabu ya hali ya juu; unyenyekevu, mazingatio kamili na kutafuta baraka za Mwenyezi Mungu. Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba neno "Salat" linaashiria kuungua kama vile kitu kiwakavyo katika moto. Hivyo, kiwango cha

Endelea uk. 11